JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NZEGA
SHULEYA SEKONDARI BUGWANGOSO
Barua pepe:bugwangososecondaryschool@gmail.com

S.L.P 256, NZEGA

Mkuu wa shule Simu Na: 0759 007 274
Makamu Mkuu wa shule Utawala: 0763 506 904
Makamu Mkuu wa shule Taaluma: 0758 626 327

Mzazi/mlezi wa mwanafunzi
…………………………………………………….
S.L.P…………………………………………….
…………………………………………………………

YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BUGWANGOSO HALMASHAURI YA MJI NZEGA, MKOA WA TABORA, MWAKA……….</u>.

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato chaTano katika shule ya sekondari bugwangoso kwa Tahasusi..........................mwaka………………………………….
2. Shule ya Sekondari Bugwangoso ipo umbali wa kilometa 3 Magharibi kutoka Stendi Kuu ya Mji wa Nzega. Usafiri wa boda boda au Bajaji unapatikana katika kituo cha mabasi NZEGA MJINI kwa nauli ya shilingi 1000/= mpaka 2000/=
3. Muhula wa masomo unaanza tarehe…………….Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni tarehe………………….tayari kwa kuanza masomo. Mwisho wa kuripoti ni tarehe…………….
4. Kumbuka kuripoti katika ofisi ya makamu mkuu wa shule mara unapoingia maeneo ya shule, hivyo utapokelewa na kusajiliwa kwenye rejesta ya shule utakapokuwa umetimiza mambo yaliyomo kwenye fomu hii na kukabidhi au kuwasilisha kivuli ( nakala picha) ya cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa pamoja na matokeo ya kidato cha nne au Result slip.

## 1.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. SARE YA SHULE
   - Mashati 2 meupe yenye mikono mirefu na mfuko upande wa kushoto.
   - Sketi 2 za lindabox (malinda madogo mawili upande wa kulia na kushoto na linda kubwa moja mbele na nyuma) vazi rasmi la darasani zenye rangi ya kaki na ziwe na urefu kuvuka magoti.
   - Flana (T-shirt) 1 yenye nembo ya shule na yenye kola (Form six) rangi nyeusi iliyoiva.
   - Gauni mbili (2) za blue zenye lindabox mbele na nyuma za kushindia ziwe ndefu zinzofika kwenye kifundo cha mguu na ashone mwenyewe
   - Juba / Shungi mbili nyeupe kwa Waislam zinazofunika kifua
   - Mwanafunzi aje na Sweta 1 rangi ya darkred (damu ya mzee) yenye shingo ya“V” mbele.
   - Tai ndefu inayoendana na rangi ya sketi.
   - Soksi nyeupe ndefu zisiwe na weusi kwenye unyayo angalau jozi 2
   - Viatu vya shule vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba jozi 2, kiwi na brashi yake
   - Track-suit moja rangi ya kijivu yenye mistari myeupe
   - Raba nyeupe pair 1

NB:HAURUHUSIWI KUJA NA NGUO NYINGINE YOYOTE ISIYO SARE YA SHULE

## 2. MICHANGO YA SHULE

a) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

(i) TSH 65,000/= kwa ajili ya mchango wa uendeshaji shule
(ii) TSH 5,000/= kwa ajili ya kitambulisho
(iii) TSH 5,000/= kwa ajili ya nembo ya Shule
(iv) TSH 5,000/= Fedha ya Tahadhari

JUMLA TSH 80,000/=

Michango ilipwe kwenye Akaunti ya shule NAMBA 51110022016 - NMB BANK, JINA LA AKAUNTI: BUGWANGOSO SEKONDARI.

NB:Kuhusu matibabu kwa wale wenye bima ya afya njoo na kadi yako na kwa ambao hawana bima ya afya watatakiwa kujiunga na mfuko wa bima ya afya (NHIF) Pindi wafikapo shule kwa gharama ya TSH 54,000.

Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

- Godoro (futi3x6) upana.
- Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko kwa ajili ya kuogea na kufulia.
- Mto1 na foronya za rangi ya pinki zisizo na maua.
- Shuka za kulalia rangi ya pinki 2, na chandarua cha pembe 4
- Nguo za ndani za kutosha na mahitaji yake muhimu.
- Faili la kuhifadhia mitihani yake.
- Vyombo vya kulia chakula (kikombe, sahani, bakuli na kijiko).
- Daftari kubwa 9 (counter books Quire 3), kalamu za wino 30 (blue), madaftari madogo dazan1na penseli dazan 1
- Mathematical set 1
- Ream 2 za A4
- Aje na vitabu vya masomo yake.
- Taulo za kike za kutosha, sabuni za kufulia na kuogea na vifaa vingine muhimu kwa matumizi yake.
- Jembe 1
- Kitenge au khanga pamoja na taulo, blanketi zito.
- Sanduku imara (trunker).
- Fyekeo1 na ufagio laini1(softbroom)
- Mopper moja
- Scientific Calculator yenye Function 991.

## 3. Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule.

4. Makosa yatakayo sababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:
   i. Wizi;
   ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
   iii. Kugombana, kuhamasisha mgomo;
   iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
   v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
   vi. Hairuhusiwi kusuka, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
   vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
   viii. Uvutaji wa sigara;
   ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
   x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
   xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
   xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
   xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
   xiv. Kudharau Bendera yaTaifa;
   xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

   Aidha, Makosa mengine ambayo hayakutajwa hapo juu mfano; kukwepa kufanya majaribio, mahudhurio hafifu darasani, kutotii kengele, kutokamilisha kazi za darasani, kutofanya usafi wa eneo ulilopangiwa, kuzungumza kiswahili ukiwa eneo la shule nk yatatolewa adhabu ndani ya shule.

   Mwanafunzi hataruhusiwa kutoka nje ya shule kutafuta huduma za kifedha au manunuzi yeyote isipokuwa kwa kusaidiwa na walimu wake walezi yaani Matron/patron

5. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU
   a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
   b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi / mkataba wa kutokushiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
   c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
   d) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na nanba zao za simu.
6. Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII



ARAFAT TENGENEZA
MKUU WA SHULE



## KUMBUKUMBU MUHIMU ZA MWANAFUNZI

A. MWANAFUNZI NA WAZAZI/WALEZI WAKE

(i) Jina la mwanafunzi.....................................................................................................

(ii) Tarehe ya kuzaliwa....................................mahali..........................................................

(iii) Jina la baba.............................................yu hai / amefariki...........................................

(iv) Mahali anakoishi;

Kijiji / Mji.............................kata............................tarafa...........................................

(v) Kazi ya baba..................................................................................................................

(vi) Anwani yake..........................................................simu..........................................

(vii) Jina la mama........................................yu hai / amefariki.............................................

(viii) Mahali anakoishi;

Kijiji / Mji............................kata.............................tarafa............................................

(ix) Kazi ya mama...............................................................................................................

(x) Anwani yake..............................................................simu......................................

(xi) Jina la mlezi.................................................................................................................

(xii) Mahali anakoishi;

Kijiji / Mji.............................kata...........................tarafa.............................................

(xiii) Anwani yake..........................................................simu.........................................

B. NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI

| NA | JINA | UHUSIANO | NA. YA SIMU |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |

C. AHADI YA KUFUATA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE (MWANAFUNZI).

Mimi ....................................................................... naahidi kufuata sheria, kanuni na taratibu za Shule hii nakutekeleza maagizo yote yatakayotolewa na uongozi wa shule wakati wote nitakao kuwa ndani na nje ya shule. Sitajihusisha na migomo, fujo wala makosa ya jinai.

Sahihi.........................................tarehe..............................................

D. AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi ........................................................................................... ambaye ni mzazi / mlezi wa mwanafunzi aliyeweka ahadi hapo juu, naahidi kumpatia michango na mahitaji yote yanayotakiwa kujiunga na shule hii.

Sahihi........................................tarehe.................................................

PRIME MINISTER'S OFFICE-REGION ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
NZEGA TOWN COUNCIL
BUGWANGOSO SECONDARY SCHOOL

# MEDICALEXAMINATIONFORM

To be completed by Government medical officers inrespect of all new entrants to Bugwangoso Secondary School.

Full name.........................................................................................

Age...........................................................

1. Blood comment (Red & White):.........................................................................................
2. Urine examination:..........................................................................................................
3. Stool examination:...........................................................................................................
4. Syphilis test:....................................................................................................................
5. T.B test:...........................................................................................................................
6. Ear test:...........................................................................................................................
7. Eye test:...........................................................................................................................
8. Spleen:..........................................................................................................................
9. Abdominal:....................................................................................................................
10. Additional information or any other physical, here ditary or infectious disease:
    .......................................................................................................................
    .......................................................................................................................
    Treatment after examination:
    .......................................................................................................................
    ..........................................................................................................................

MEDICALCERTIFICATE

I certify that the above mentioned has been examined and found fit / unfit to pursue further education.

Signature......................................................

Designation..................................................

Station..........................................................

(Officials tamp).................................

Date.............................................................

NB:Fomu hii ijazwe na Mganga katika hospitali ya Serikali au inayotambulika na Serikali